**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 987

Jina la Chapisho: Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV
Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania
Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
ISBN: 978-9987-09-824-8

Mtaala huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MTAALA WA ELIMU YA SEKONDARI
# KIDATO CHA I - IV

**2023**

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza 2023

ISBN: 978-9987-09-824-8

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es salaam

Simu: +255 735 041 168/ +255 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Mtaala huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

## Yaliyomo

**Orodha ya Majedwali** ... v

**Vifupisho** ... vi

**Shukurani** ... vii

**Dibaji** ... viii

**Sehemu ya Kwanza** ... 1

**Utangulizi** ... 1

1.1 Usuli ... 1

1.2 Muundo wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV ... 1

**Sehemu ya Pili** ... 3

**Dira, Malengo na Umahiri wa Jumla** ... 3

2.1 Dira ya Elimu ya Tanzania ... 3

2.2 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania ... 3

2.3 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV Elimu ya Jumla ... 3

2.4 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV Elimu ya Amali ... 4

2.5 Umahiri wa Jumla - Elimu ya Jumla ... 4

2.6 Umahiri wa Jumla - Elimu ya Sekondari Mkondo wa Amali ... 5

**Sehemu ya Tatu** ... 6

**Maudhui ya Mtaala** ... 6

3.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo - Elimu ya Jumla ... 6

3.2 Fani Kuu na Fani Mahusuhi - Elimu ya Amali ... 8

3.3 Masomo yatakayosomwa katika mkondo wa Elimu ya Amali ... 13

3.4 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi - Elimu ya Jumla ... 16

**Sehemu ya Nne** ........ 44

**Ufundishaji na Ujifunzaji** ........ 44

4.1 Masuala Mtambuka........ 44
4.2 Muda na Idadi ya Vipindi........ 44
4.3 Lugha ya Kufundishia na Kujifunzia. ........ 46

**Sehemu ya Tano** ........ 47

**Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji na Ujifunzaji**........ 47

5.1 Upimaji wa Masomo ya Taaluma ........ 47
5.2 Upimaji wa Fani za Elimu ya Amali ........ 50

**Sehemu ya Sita**........ 51

**Rasilimali za Utekelezaji wa Mtaala**........ 51

6.1 Rasilimali Watu ........ 51
6.2 Rasilimali Vitu ........ 51
6.3 Samani na Majengo ........ 52
6.4 Rasilimali Muda........ 52
6.5 Rasilimali Fedha ........ 52
6.6 Ushiriki wa Wadau katika Utekelezaji wa Mtaala ........ 52
6.7 Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Mtaala........ 53

**Bibliografia**........ 54

**Orodha ya Majedwali**

Jedwali Na.1: Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo ........................................................ 6

Jedwali Na. 2: Fani kuu na fani mahususi.................................................................... 8

Jedwali Na. 3: Masoma Yatakayofundishwa Mkondo wa Amali .............................. 13

Jedwali Na. 4: Somo, Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ..................................... 16

Jedwali Na. 5: Masomo ya Msingi na Lazima na Idadi ya Vipindi kwa Wiki ........... 45

Jedwali Na. 6: Masomo Chaguzi na Idadi ya Vipindi kwa Wiki................................. 45

Jedwali Na 7: Mgawanyo wa Muda kwa Mkondo wa Elimu ya Amali.......................46

Jedwali Na. 8: Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu na Tamati kwa Masomo Yaliyoanza Kufundishwa Darasa la III.....................................48

Jedwali Na. 9: Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu kwa Masomo Yanayoanza Kufundishwa Kidato cha I....................................................49

Jedwali Na.10: Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu na Tamati kwa Masomo Yanayoanza Kufundishwa Kidato cha III............................49

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| LAT | Lugha ya Alama ya Tanzania |
| NACTVET | National Council for Technical and Vocational Education and Training |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| TEHAMA | Teknoljia ya Habari na Mawasiliano |
| WyEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| SADC | Southern Africa Development Community |

## Shukurani

Maandalizi ya Mtaala huu yamehusisha wadau mbalimbali kutoka sekta za umma na binafsi. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha upatikanaji wa Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I-IV. Hivyo, TET inatoa shukurani za dhati kwanza, kwa Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda (Mb.). Kamati hiyo ilikuwa na wajumbe kumi (10), wakiongozwa na Mwenyekiti wake Prof. Makenya Abraham Maboko. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi kuhakikisha kuwa mtaala huu unaandaliwa kwa wakati na unakidhi shauku ya wadau juu ya ubora wa elimu ya sekondari.

Pili, shukurani ziende kwa Taasisi, Wizara na wadau mbalimbali wa elimu walioshiriki kutoa maoni kuhusu uboreshaji wa mtaala. Baadhi ya Taasisi, Wizara na wadau hao ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wajumbe wa Kamati ya Mapitio ya Sera ya Elimu, wajumbe wa Kamati ya Kufanya Mageuzi Makubwa ya Elimu Zanzibar, viongozi wa dini, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Taasisi ya Elimu Zanzibar, Bodi na Menejimenti za Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Tanzania, Menejimeti na Wakufunzi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, Chuo cha Amali Zanzibar, Baraza la Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi, Baraza la Mitihani Tanzania, Chama cha Walimu Tanzania na Baraza la Watoto na Vijana Balehe Tanzania. Vilevile, wadau wengine ni wajumbe wa bodi za shule, wanafunzi wa shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu, walimu wa shule za msingi, sekondari, wakufunzi wa vyuo vya ualimu, wahadhiri wa vyuo vikuu, waajiri, wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu, Tume ya Vyama vya Ushirika, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Akademia ya Sayansi Tanzania, Benki Kuu ya Tanzania na Shirika la Chakula na Kilimo la Kimataifa.

Tatu, TET inayashukuru mashirika ya *United Nations Children's Fund*, *United Nations Educational, Scientific and Cultural Organisation, Room to Read, Right to Play, Data Vision, Plan International, Norwegian Refugees Council, Christian Social Services Commission, Global Education Link,* UWEZO, *Hill Packaging Ltd., Teacher Education Support Project, Madrasa Early Childhood Programme – Zanzibar, Morale Foundation for Education and Training* na *Educate!* kwa kufadhili hatua mbalimbali za uandaaji wa mtaala huu.

Nne, TET inatoa shukurani za dhati kwa wataalamu wote wa elimu ya sekondari kutoka ndani na nje ya TET walioshiriki kuandaa mtaala huu. Mwisho, TET inaishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) kwa kuwezesha kazi ya uandishi, uchapaji na usambazaji wa mtaala huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## Dibaji

Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV umeandaliwa kwa kuzingatia *Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014* Toleo la Mwaka 2023, maoni ya wadau yaliyokusanywa na kuchakatwa kati ya mwaka 2021 na 2022 na matokeo ya uchambuzi wa maandiko kuhusu uzoefu kutoka nchi nyingine. Mtaala huu unazingatia dira ya elimu inayolenga kumwandaa Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo katika kuleta maendeleo endelevu ya kitaifa na kimataifa. Aidha, Mtaala huu umezingatia malengo makuu ya elimu pamoja na malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV. Kwa kuzingatia haya, mtaala huu umeweka viwango vya utoaji wa elimu katika ngazi ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV kwa kubainisha ujuzi, maarifa, stadi na mwelekeo atakaoujenga mwanafunzi, umahiri wa jumla, maeneo makuu ya ujifunzaji, umahiri mkuu na mahususi na njia za ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, mtaala umebainisha muda utakaotumika katika utekelezaji, lugha ya kujifunzia na kufundishia, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na njia zitakazotumika kupima maendeleo ya mwanafunzi kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri. Vilevile, mtaala umebainisha sifa za kitaaluma na kitaalamu za mwalimu ambaye ndiye mtekelezaji mkuu wa mtaala katika ngazi ya shule.

Pamoja na matamko mbalimbali ya kisera na miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa, mtaala huu umezingatia nadharia za ujifunzaji na Falsafa ya Eimu ya Kujitegemea inayosisitiza utoaji wa elimu inayomwezesha Mtanzania kujitegemea na kumudu maisha yake ya kila siku. Hivyo, utekelezaji wake utawezesha ukuaji wa mwanafunzi kimwili, kiakili, kihisia na kijamii. Ni matarajio yangu kuwa kupitia mtaala huu, mwalimu atamwezesha mwanafunzi kujenga umahiri uliokusudiwa. Pia, wasimamizi wote wa utekelezaji wa mtaala na wadau wengine wa Elimu ya Sekondari nchini watahakikisha kuwa elimu inayotolewa inakidhi viwango vya ubora vinavyokubalika kitaifa, kikanda na kimataifa.



Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
**Kamishna wa Elimu**

## Sehemu ya Kwanza

## Utangulizi

### 1.1 Usuli

Nchi nyingi duniani, ikiwemo Tanzania, zinatambua kwamba elimu ni haki ya kila mtoto na hivyo zimekuwa zikifanya jitihada mbalimbali ili kuhakikisha kuwa elimu bora inatolewa kwa haki na usawa. Jitihada hizi zinafanyika kutokana na ukweli kwamba elimu ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya kila mtoto kitaaluma, kimaadili na katika ukuzaji wa vipaji na vipawa mbalimbali. Kutokana na azma ya Taifa ya kujenga nchi yenye uchumi shindani kitaifa, Serikali imelenga kujenga jamii yenye maarifa, stadi na mwelekeo chanya itakayoweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za kimaendeleo. Pamoja na azma hiyo, Tanzania imeridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika yaani *Southern Africa Development Community (SADC)* ya mwaka 1997 kuhusu elimu na mafunzo inayozitaka nchi wanachama kuwa na elimu ya lazima kwa kipindi kisichopungua miaka tisa.

Tanzania imejizatiti kutoa elimu bora na jumuishi inayozingatia Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea iliyoasisiwa mwaka 1967 na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Aidha, Mtaala huu umejikita katika ujenzi wa umahiri wa msingi katika Stadi za Karne ya 21 ambazo ni kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi, utatuzi wa matatizo na ujuzi wa kidigiti. Hivyo basi, Mtaala huu umeandaliwa kwa lengo la kuwandaa Watanzania wenye maarifa, maadili, uzalendo, stadi na mtazamo chanya katika kuchangia maendeleo ya Taifa kwa kuzingatia mabadiliko ya sayansi na teknolojia na mahitaji ya Karne ya 21. Uandaaji wa mtaala huu umepitia hatua mbalimbali ikiwemo; kukusanya maoni ya wadau, mapitio ya nyaraka mbalimbali na kujifunza uzoefu kutoka nchi mbalimbali kwa lengo la kujifunza mifano bora inayoweza kutekelezeka katika mazingira ya Tanzania.

### 1.2 Muundo wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV

Kama inavyoelekezwa na *Sera ya Elimu na Mafunzo 2014* Toleo la Mwaka 2023, Elimu ya Sekondari Kidato cha I-IV itadumu kwa muda wa miaka minne (4). Elimu hii imegawanyika katika mikondo miwili: Mkondo wa Elimu ya Jumla na Mkondo wa Elimu ya Amali. Mwanafunzi atachagua mkondo kulingana na matakwa, uwezo na malengo yake ya maisha.

Mkondo wa Elimu ya Jumla umegawanyika katika michepuo kumi na moja (11) ambayo ni Sayansi, Kilimo, Michezo, TEHAMA, Biashara, Muziki, Sayansi ya Jamii, Sanaa, Ushoni, Chakula na Lishe na Lugha. Aidha, kuanzia Kidato cha I mwanafunzi atachagua masomo katika moja ya michepuo kulingana na matakwa, uwezo na malengo yake ya maisha. Licha ya masomo katika michepuo yao, wanafunzi wote wa Mkondo wa Elimu ya Jumla wataweza kuchagua masomo ya ziada, yakiwamo yale ya Mkondo wa Elimu ya Amali, kulingana na ratiba na uwezo wa shule husika.

Mkondo wa Elimu ya Amali umegawanyika katika Fani Kuu (*Main Fields*) kumi na tano (15) ambazo ni Uhandisi Umeme (*Electrical Engineering),* Uhandisi Mitambo *(Mechanical Engineering),* Uhandisi Ujenzi *(Civil Engineering),* Uhandisi Magari *(Automotive Engineering),* Huduma za Usafirishaji *(Transport and Logistics),* Ushoni *(Clothing and Textile),* Kilimo, Ufugaji na Usindikaji Vyakula (*Agriculture and Food Processing),* Utalii *(Hospitality and Tourism),* Huduma Saidizi za Biashara *(Commercial and Business Support Services), Uchapishaji (Printing),* Uchimbaji na Uchenjuaji Madini *(Extraction and Processing of Minerals),* Urembo na Ususi *(Cosmetology),* Sanaa Bunifu *(Creative Arts),* Elektroniki na Kompyuta *(Electronics and Computer*) na Michezo (*Sports).* Aidha, kila fani kuu ina fani mahususi kadhaa.

Kuanzia Kidato cha I mwanafunzi atachagua fani mahususi moja kulingana na matakwa yake, uwezo na malengo yake ya maisha. Wanafunzi wote wa mkondo wa Elimu ya Amali watalazimika kusoma masomo ya lazima manne (4) ambayo ni Hisabati, Elimu ya Biashara, *English Language* na Historia ya Tanzania na Maadili. Masomo ya ufundi yatafundishwa kwa mfumo wa moduli. Mwanafunzi akikamilisha idadi ya moduli ya fani aliyosoma na kufaulu atatunukiwa Tuzo ya Taifa ya Ufundi Stadi (National Vocational Awards-NVA) kulingana na ngazi husika. Wanafunzi wote wa Kidato cha I na II wa Elimu ya Amali watasoma maudhui ya NVA Ngazi ya 1 Kidato cha III atasoma maudhui ya NVA Ngazi ya 2 na Kidato cha IV atasoma maudhui ya NVA Ngazi ya 3.

Mwanafunzi ataanza Kidato cha I akiwa na umri wa miaka 12 na kuhitimu Kidato cha IV akiwa na umri wa miaka 15.

## Sehemu ya Pili

## Dira, Malengo na Umahiri wa Jumla

Mtaala huu umezingatia dira, malengo na umahiri unaotakiwa kujengwa kwa kila hatua ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV.

### 2.1 Dira ya Elimu ya Tanzania

Kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo katika kuleta maendeleo endelevu ya kitaifa na kimataifa.

### 2.2 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

### 2.3 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV Elimu ya Jumla

Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV Elimu ya Jumla ni:

(a) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, stadi na mwelekeo alioupata katika hatua ya Elimu ya Msingi;

(b) Kulinda mila na desturi, umoja wa kitaifa, tunu za taifa, demokrasia, kuthamini haki za binadamu na za kiraia, wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo;

(c) Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, na kiufundi;

(d) Kuimarisha mawasiliano kwa kutumia stadi za lugha ikiwemo Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha mguso, lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Aidha, mwanafunzi ahamasishwe kumudu angalau lugha nyingine moja ya kigeni kulingana na hali halisi ya shule yake;

(e) Kuimarisha uwajibikaji katika masuala mtambuka ya kijamii yakiwemo afya, usalama, usawa wa kijinsia na utunzaji endelevu wa mazingira;

(f) Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake, na

(g) Kukuza utayari wa kujiendeleza na mafunzo ya elimu ya kati na ya juu.

## 2.4 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV Elimu ya Amali

Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I-IV Elimu ya Amali ni:

(a) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, stadi, na mwelekeo alioupata katika hatua ya elimu ya msingi;

(b) Kukuza stadi za ufundi na ujasiriamali zitakazomwezesha kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake;

(c) Kulinda mila na desturi, umoja wa kitaifa, tunu za taifa, demokrasia, kuthamini haki za binadamu na za kiraia, wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo;

(d) Kuimarisha mawasiliano kwa kutumia stadi za lugha;

(e) Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, na kiufundi;

(f) Kuimarisha uwajibikaji katika masuala mtambuka ya kijamii yakiwemo afya, usalama, usawa wa kijinsia, na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(g) Kukuza utayari wa kujiendeleza na mafunzo ya Elimu ya Amali na sanifu, au Sekondari hatua ya juu.

## 2.5 Umahiri wa Jumla - Elimu ya Jumla

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwanafunzi wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV Elimu ya Jumla ni:

(a) Kutumia maarifa na stadi alizozipata katika hatua ya elimu ya msingi kuimarisha na kupanua uelewa wa kitaaluma;
(b) Kuthamini uraia na tunu za taifa;
(c) Kuonesha kujiamini katika kujifunza nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia na kivitendo;
(d) Kutumia stadi za lugha ikiwemo Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha mguso, lugha ya Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha moja nyingine ya kigeni kuwasiliana;
(e) Kutumia maarifa ya masuala mtambuka kuyamudu mazingira yanayomzunguka; na
(f) Kutumia ujuzi na stadi kumwezesha mwanafunzi kujiajiri, kuajiriwa na kuyamudu maisha na mazingira yanayomzunguka.

### 2.6 Umahiri wa Jumla - Elimu ya Sekondari Mkondo wa Amali

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwanafunzi wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV Mkondo wa Amali ni:

(a) Kutumia maarifa, stadi na mwelekeo alioupata hatua ya elimu ya msingi ili kukuza uelewa wa stadi za ufundi;
(b) Kutumia stadi za ufundi katika kubuni, kuvumbua na kutengeneza vitu mbalimbali ili kuyamudu maisha na kutatua changamoto katika jamii;
(c) Kuthamini uraia na tunu za taifa;
(d) Kutumia stadi za lugha;
(e) Kuonesha kujiamini katika ujifunzaji katika nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa na stadi za ufundi;
(f) Kutumia maarifa na stadi za ufundi katika kubuni, kugundua na kutengeneza vitu mbalimbali ili kutatua changamoto katika jamii yakiwemo masuala mtambuka;
(g) Kuthamini taratibu na kanuni za usalama katika kutumia zana za ufundi kwa usahihi; na
(h) Kutumia maarifa na stadi za ufundi alizozipata ili kujiendeleza na mafunzo ya Elimu ya Amali na sanifu na kuingia katika kazi.

## Sehemu ya Tatu

## Maudhui ya Mtaala


Sehemu hii inafafanua maeneo ya ujifunzaji na masomo kwa Elimu ya Sekondari Kidato I – IV. Elimu ya Jumla, Fani kuu na mahususi kwa Elimu ya Amali na Umahiri mkuu na mahususi wa masomo mbalimbali.

### 3.1 Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo - Elimu ya Jumla

Maeneo ya ujifunzaji na masomo katika hatua hii yamefafanuliwa katika Jedwali Na. 1. Aidha, michepuo na masomo vimefafanuliwa katika Kielelezo Na. 1.

**Jedwali Na.1:** *Maeneo ya Ujifunzaji na Masomo*

| Na | Maeneo ya ujifunzaji | Masomo |
|---|---|---|
| 1 | Sayansi Asilia, Teknolojia na Mazingira | 1. Baiolojia<br>2. Fizikia<br>3. Kemia<br>4. Kilimo<br>5. Sayansi ya Kompyuta |
| 2 | Sayansi Jamii, Imani na Maadili | 1. Jiografia<br>2. Historia ya Tanzania na Maadili<br>3. Historia<br>4. Elimu ya Dini ya Kikristo<br>5. Elimu ya Dini ya Kiislamu |
| 3 | Hisabati | 1. Hisabati<br>2. Addi*tional Mathematics* |
| 4 | Lugha na Mawasiliano | 1. Kiswahili<br>2. *English language*<br>3. Kichina<br>4. Kiarabu<br>5. Kifaransa<br>6. *Literature in English*<br>7. Fasihi ya Kiswahili |
| 5 | Elimu ya Amali, Ujasiriamali na Uchumi | 1. Elimu ya Biashara<br>2. Utunzaji wa Taarifa za Fedha<br>3. Ushoni<br>4. Chakula na Lishe |
| 6 | Utamaduni, Sanaa na Michezo | 1. Muziki<br>2. Michezo<br>3. Sanaa Sanifu<br>4. Sanaa za Maonyesho |




**Kielelezo Na. 1:** *Michepuo na masomo*

### 3.2 Fani kuu na Fani mahusuhi - Elimu ya Amali

Fani kuu na mahususi kwa Elimu ya Amali zimeainishwa katika Jedwali Na. 2 na Kielelezo Na. 2.


**Jedwali Na. 2:** *Fani kuu na fani mahususi*

| Na | Fani Kuu | Fani mahususi |
|---|---|---|
| 1. | Electrical Engineering | 1.1 Electrical installation |
| | | 1.2 Bio-energy installation |
| | | 1.3 Wind power plants installation |
| | | 1.4 Solar power installation |
| 2. | Mechanical Engineering | 2.1 Welding and metal fabrication |
| | | 2.2 Refrigeration and air conditioning |
| | | 2.3 Fitter machinist |
| | | 2.4 Fitter mechanics |
| | | 2.5 Ginnery fitting |
| 3. | Civil Engineering | 3.1 Masonry and brick-laying |
| | | 3.2 Civil drafting |
| | | 3.3 Boat building |
| | | 3.4 Carpentry and joinery with metal works |
| | | 3.5 Plumbing and pipe fitting |
| | | 3.6 Painting and sign writing |
| | | 3.7 Steel fixing |
| | | 3.8 Well drilling |
| | | 3.9 Wood carving |
| 4. | Automotive Engineering | 4.1 Motor vehicle mechanics |
| | | 4.2 Auto-electric mechanics |
| | | 4.3 Auto-body repair |

| Na | Fani Kuu | Fani mahususi |
|---|---|---|
| | | 4.4 Motor-cycle mechanics |
| | | 4.5 Agro-mechanics |
| 5. | Electronics and Computer | 5.1 Computer programming |
| | | 5.2 Graphics design |
| | | 5.3 Electronics Repair |
| | | 5.4 Computer maintenance |
| | | 5.5 Mobile phone repair |
| | | 5.6 Office machines maintenance |
| | | 5.7 Film and TV Production |
| 6. | Transport and Logistics | 6.1 Transport operations |
| | | 6.2 Clearing and forwarding |
| 7. | Clothing and Textile | 7.1 Handloom weaving |
| | | 7.2 Finishing craft |
| | | 7.3 Basic knitting |
| | | 7.4 Designing, sewing and cloth technology |
| | | 7.5 Leather goods and footwear |
| 8. | Agriculture and Food Processing | 8.1 Meat processing and technology |
| | | 8.2 Oil seed processing |
| | | 8.3 Animal health and production |
| | | 8.4 Horticulture production |
| | | 8.5 Field crop production |
| | | 8.6 Wood processing |
| | | 8.7 Bee keeping |
| | | 8.8 Fishing and fish processing |
| | | 8.9 Aquaculture and fish processing |
| | | 8.10 Seaweed farming |

| Na | Fani Kuu | Fani mahususi |
|---|---|---|
| 9. | Hospitality and Tourism | 9.1 Front office operations |
| | | 9.2 House-keeping |
| | | 9.3 Food production |
| | | 9.4 Food beverage services and sales |
| | | 9.5 Tour guide and travel operations |
| 10. | Commercial and Business Support Services | 10.1 Business operation assistance |
| | | 10.2 Secretarial |
| | | 10.3 Insurance |
| | | 10.4 Wholesale and retailing |
| | | 10.5 Geospatial technology |
| 11. | Printing | 11.1 Packaging printing |
| | | 11.2 Screen printing |
| | | 11.3 Binding and print finishing |
| 12. | Extraction and Processing of Minerals | 12.1 Jewellery |
| | | 12.2 Salt extraction |
| | | 12.3 Gemology (Gemstone cutting, polishing and carving) |
| 13. | Cosmetology | 13.1 Hair dressing |
| | | 13.2 Beauty therapy |
| | | 13.3 Fitness and nutrition |
| 14. | Creative Arts | 14.1 Acting |
| | | 14.2 Costume and makeup designs |
| | | 14.3 Ngoma performance |
| | | 14.4 Music and sound technology |
| | | 14.5 Music performance |
| | | 14.6 Carving |

| Na | Fani Kuu | Fani mahususi |
|---|---|---|
| | | 14.7 Drawing and painting |
| | | 14.8 Pottery and ceramic |
| | | 14.9 Textile design and small-scale Printing |
| | | 14.10 Art and design |
| 15. | Sports | 15.1 Football perfomance |
| | | 15.2 Netball perfomance |
| | | 15.3 Track events |




**Kielelezo Na. 2:** *Michepuo ya Fani Mbalimbali za Mkondo wa Elimu ya Amali*

### 3.3 Masomo yatakayo somwa katika mkondo wa Elimu ya Amali

**Jedwali Na. 3.** *Masomo yatakayofundishwa mkondo wa Amali*

| Na | Fani Kuu | Masomo yatakayo fundishwa kwa kutumia Mtaala wa VETA | Masomo yatakayo fundishwa kwa kutumia Mtaala wa TET |
|---|---|---|---|
| 1. | **Amali za Kihandisi** (Electrical Installation, Motor Vehicle Mechanics; Welding and Metal Fabrication; Painting and Sign Writing; Carpentry and Joinery with Metal work; Masonry and Brick Laying; Plumbing and Pipe Fitting; and Solar Power Installation) | Somo fani | Mathematics |
| | | Technical Drawing | Business Studies |
| | | Computer Application with CAD | English Language |
| | | Life Skills | Historia ya Tanzania na Maadili |
| | | | Engineering Science |
| 2. | **Amali za Ukarimu na Utalii** (Food Production; Food and Beverages Services; House Keeping; Front Office Operations; Tour Guide) | Somo fani | Historia ya Tanzania na Maadili |
| | | Tourism for Hospitality | English Language |
| | | Life Skills | French Language |
| | | Computer applications | Mathematics |
| | | | Business Studies |
| 3. | **Amali za Kilimo na Mifugo** (Field Crop Production; Horticulture, Animal Health and Production, Meat Processing) | Somo fani | Mathematics |
| | | Computer Application | Agriculture |
| | | Life Skills | Business Studies |
| | | | English Language |
| | | | Historia ya Tanzania na Maadili |
| | | | Biology |

| Na | Fani Kuu | Masomo yatakayo fundishwa kwa kutumia Mtaala wa VETA | Masomo yatakayo fundishwa kwa kutumia Mtaala wa TET |
|---|---|---|---|
| 4. | **Amali za Sanaa na Maonyesho** (Music Performance, Music Sound and Technology, Acting, Ngoma) | Somo fani | Historia ya Tanzania na Maadili |
| | | Computer Application | Mathematics |
| | | Life Skills | English Language |
| | | | Bussiness Studies |
| | | | Chinese language / French language /Arabic language* |
| 5. | **Amali za Michezo** (Football, Netball, Track Event) | Somo fani | Historia ya Tanzania na Maadili |
| | | Computer Application | Mathematics |
| | | Life Skills | English Language |
| | | | Business Studies |
| | | | Chinese language / French language /Arabic language* |
| 6. | **Amali za TEHAMA** Film and TV Production, Office Machines Maintenance, Mobile Phone Repair and Computer Maintenance) | Somo fani | Mathematics |
| | | Computer applications | English Language |
| | | Life Skills | Business Studies |
| | | | Historia ya Tanzania na Maadili |
| | **Amali za TEHAMA** (Graphic Design, Computer Programming, | Somo la Fani | Mathematics |
| | | Computer application with CAD | English Language |
| | | Life Skills Technical Drawing | Business Studies |
| | | | Historia ya Tanzania na Maadili |
| | | | Engineering Science |

| Na | Fani Kuu | Masomo yatakayo fundishwa kwa kutumia Mtaala wa VETA | Masomo yatakayo fundishwa kwa kutumia Mtaala wa TET |
|---|---|---|---|
| 7. | **Amali za Ushoni** (Leather Goods and Foot Wear, Design Sewing and Cloth Technology, Handloom and Weaving) | Somo fani | Historia ya Tanzania na Maadili |
| | | Technical Drawing | English Language |
| | | Computer application with CAD | Mathematics |
| | | Life skills | Business studies |
| | | | Engineering science |

*Mwanafunzi anaruhusiwa kuchagua somo moja

### 3.4 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi - Elimu ya Jumla

Umahiri mkuu na mahususi wa Kidato cha I - IV Elimu ya Jumla wa kila somo umeainishwa katika Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na. 4:** *Somo, Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi*

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| 1 | Historia ya Tanzania na Maadili | 1.1 Kulinda historia, urithi na maadili ya Taifa | 1.1.1 Kuelezea chimbuko la jamii za Kitanzania na maadili yake<br>1.1.2 Kumudu maarifa na ujuzi wa maadili na urithi wa jamii za Kitanzania<br>1.1.3 Kutumia maarifa na ujuzi wa historia na urithi kubuni fursa mbalimbali zilizopo katika jamii za Kitanzania<br>1.1.4 Kubaini fursa mbalimbali za kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa kitaifa |
| | | 1.2 Kumudu historia ya jamii za Kitanzania na maadili yake kabla ya ukoloni | 1.2.1 Kuchambua mifumo ya kijamii (elimu, afya, utamaduni, uchumi) iliyokuza na kuendeleza maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni<br>1.2.2 Kuchambua mifumo iliyokuza na kuendeleza uchumi na siasa katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni<br>1.2.3 Kutathmini vichocheo vya mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
| --- | --- | --- | --- |
| | | 1.3 Kumudu historia ya Tanzania na maadili wakati wa ukoloni, 1890- 1960 | 1.3.1 Kutumia maarifa na ujuzi wa chimbuko na ukuaji wa mfumo wa ukoloni kuelewa uhusiano wa kihistoria kati ya Tanzania na mataifa yaliyoitawala<br>1.3.2 Kutathmini athari za mfumo wa ukoloni kwenye maadili ya jamiii za Kitanzania<br>1.3.3 Kuchambua jitihada za jamii za Kitanzania kupinga ukoloni na maadili ya kikoloni |
| | | 1.4 Kumudu historia ya ujenzi wa Taifa la Tanzania na maadili katika kipindi cha 1961-1966 | 1.4.1 Kuchambua mifumo ya uchumi, siasa, utamaduni jamii na maadili iliyojengwa 1961-1966<br>1.4.2 Kumudu historia ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar<br>1.4.3 Kumudu historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar |
| | | 1.5 Kutathmini ujenzi wa Taifa na maadili baada ya Azimio la Arusha, 1967-1985 | 1.5.1 Kuchambua chimbuko la Azimio la Arusha na matokeo yake kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kimaadili<br>1.5.2 Kueleza nafasi ya Tanzania katika kujenga uhusiano wa kikanda |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | 1.6 Kutathmini historia ya Tanzania na maadili wakati wa uliberali, 1986 hadi sasa | 1.6.1 Kuchambua chimbuko la uliberali na utandawazi<br>1.6.2 Kuishi maadili mema ya Kitanzania wakati wa uliberali na utandawazi |
| | | 1.7 Kufanya utafiti wa historia na maadili ya Tanzania | 1.7.1 Kumudu misingi ya utafiti wa kihistoria<br>1.7.2 Kutumia misingi ya utafiti wa kihistoria kufanya kazimradi |
| | | 1.8 Kumudu muundo na kazi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 1.8.1 Kueleza muundo na kazi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar<br>1.8.2 Kubaini muundo na kazi za serikali za mitaa |
| 2. | Historia | 2.1 Kumudu historia ya Afrika kabla ya ukoloni | 2.1.1 Kuelezea dhana na vyanzo vya historia<br>2.1.2 Kuchambua nadharia kuhusu asili ya binadamu<br>2.1.3 Kutathmini maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiteknolojia katika Afrika<br>2.1.4 Kuchambua mwingiliano baina ya jamii za Kiafrika<br>2.1.5 Kuchambua uhusiano kati ya Afrika, Mashariki ya Kati, Mashariki ya Mbali na Ulaya kuanzia Karne ya Kwanza hadi ya Kumi na tisa |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | 2.2 Kumudu historia ya uhusiano kati ya ubepari na Afrika | 2.2.1 Kuelezea ukuaji wa mfumo wa ubepari na athari zake kwa Afrika<br>2.2.2 Kuchambua mifumo ya kikoloni katika Afrika<br>2.2.3 Kuchambua harakati za ukombozi wa Afrika |
| | | 2.3 Kumudu historia ya ujenzi wa Afrika baada ya uhuru | 2.3.1 Kumudu historia ya ujenzi wa Afrika baada ya uhuru<br>2.3.2 Kutathmini mafanikio na changamoto katika ujenzi wa Afrika baada ya uhuru |
| | | 2.4 Kutathmini historia ya Afrika katika masuala ya kikanda na kimataifa | 2.4.1 Kuelezea historia ya uundwaji wa uhusiano wa kikanda ndani ya Afrika<br>2.4.2 Kutathmini uhusiano wa Afrika na Umoja wa Mataifa |
| 3. | Jiografia | 3.1 Kumudu stadi za muundo wa dunia | 3.1.1 Kufafanua dhana ya maumbile ya dunia na vitu vilivyomo<br>3.1.2 Kuchambua sura ya nchi<br>3.1.3 Kuhusianisha sura ya nchi, hali ya hewa na uoto wa asili |
| | | 3.2 Kumudu stadi za kijiografia | 3.2.1 Kufafanua dhana ya ramani na picha<br>3.2.2 Kumudu stadi za awali za usorovea |
| | | 3.3 Kumudu stadi za jiografia ya binadamu | 3.3.1 Konesha uelewa wa uhusiano kati ya jiografia, mtawanyiko wa watu, shughuli za kiuchumi na afya ya mazingira |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
| --- | --- | --- | --- |
| | | | 3.3.2 Kufanya kazi mradi kwa kutumia misingi ya kijiografia |
| 4 | English | 4.1 Manage information search from different sources for lifelong learning | 4.1.1 Use ICT tools to search for information from different sources<br>4.1.2 Organize information obtained from different sources |
| | | 4.2 Demonstrate mastery of English language skills | 4.2.1 Develop listening skills<br>4.2.2 Produce short and coherent oral messages with intelligible pronunciation and fluency<br>4.2.3 Develop vocabulary from conversations and written texts<br>4.2.4 Use appropriate grammar and vocabulary in oral and in written language tasks |
| | | 4.3 Comprehend oral and written information | 4.3.1 Read texts for comprehension<br>4.3.2 Comprehend oral messages with increasing difficulty<br>4.3.3 Respond appropriately in a variety of oral and written communication contexts<br>4.3.4 Construct meaning from a variety of text |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | 4.4 Communicate effectively in different contexts | 4.4.1 Use appropriate grammar and vocabulary for oral communication in a variety of contexts<br>4.4.2 Create a variety of texts for different communicative purposes using the appropriate tone and register<br>4.4.3 Conduct a socio-cultural analysis of functional texts |
| | | 4.5 Provide basic English language services to the community | 4.5.1 Apply principles of editing and proofreading in a variety of texts<br>4.5.2 Apply principles of interpretation to provide simple authentic interpretations<br>4.5.3 Apply principles of translation to produce simple authentic translation<br>4.5.4 Manage short translation and editing projects using Computer-Assisted Tools |
| | | 4.6 Appreciate and create literary works | 4.6.1 Appreciate the aesthetics and value of literature<br>4.6.2 Evaluate the context in which literary texts are written, read and understood |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | | 4.6.3 Analyse genres of literature and appreciate their conventions<br>4.6.4 Create simple literary works |
| 5 | Literature in English | 5.1 Develop awareness of and empathy with national and global literary works | 5.1.1 Demonstrate empathy for other people's experiences nationally and globally<br>5.1.2 Appreciate multiculturalism and develop self-consciousness<br>5.1.3 Reflect values, perspectives and identities, and the impact of beliefs and actions on society |
| | | 5.2 Appreciate different implications and layers of meaning in literary works | 5.2.1 Appreciate the use of literary devices in the works of art<br>5.2.2 Apply critical thinking when reading, discussing and writing about literary texts<br>5.2.3 Justify interpretations based on evidence and logic |
| | | 5.3 Compose literary works | 5.3.1 Synthesise literary characteristics, themes, and/ or approaches in several literary texts |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | | 5.3.2 Recognise ambiguity and uncertainty as necessary in creating literary works<br>5.3.3 Create imaginative and original literary works |
| 6 | Kiswahili | 6.1 Kumudu misingi ya Kiswahili | 6.1.1 Kutambua Kiswahili kama kielelezo cha utaifa na utambulisho wa Mtanzania<br>6.1.2 Kukuza uelewa wa sarufi ya Kiswahili |
| | | 6.2 Kumudu lugha ya mazungumzo na ya maandishi | 6.2.1 Kusikiliza na kuelewa mazungumzo<br>6.2.2 Kusoma matini kwa ufasaha na ufahamu |
| | | 6.3 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 6.3.1 Kutumia kamusi katika miktadha mbalimbali<br>6.3.2 Kuwasiliana kwa ufasaha kwa njia ya mazungumzo<br>6.3.3 Kuwasiliana kwa njia ya maandishi katika miktadha mbalimbali |
| | | 6.4 Kuthamini kazi za fasihi ya Kiswahili | 6.4.1 Kukuza uelewa wa misingi ya fasihi ya Kiswahili<br>6.4.2 Kuhakiki kazi za fasihi ya Kiswahili<br>6.4.3 Kubuni kazi za fasihi ya Kiswahili |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
| --- | --- | --- | --- |
| | | 6.5 Kutoa huduma ya lugha ya Kiswahili katika jamii | 6.5.1 Kufanya tafsiri sahili katika lugha ya Kiswahili<br>6.5.2 Kuhariri matini mbalimbali za Kiswahili<br>6.5.3 Kufanya ukalimani sahili kwa lugha ya Kiswahili |

| الرقم | المادة | الكفاءات العامة | الكفاءات الخاصة |
| --- | --- | --- | --- |
| 7. | اللغة العربية | 7.1 إظهار فهم المـهـارات الأساسية للغة العربية | 7.1.1 تطوير مـهـارات الاستماع اللغة العربية |
| | | | 7.1.2 اكتساب المفردات من المحادثة والكتـابة |
| | | | 7.1.3 توصيل المعلومات الفصيحة القصيرة المنطوقة بكلمات فصيحة |
| | | | 7.1.4 استخدام المفردات والقواعد الصحيحة عن طريق التحدث والكتابة |
| | | 7.2 إظهار فهم المعلومات المعروضة شفويا وكتـابيا | 7.2.1 تطوير كـفـاءة الاستماع وفهم المعلومات المعروضة شفويا |
| | | | 7.2.2 تطوير كـفـاءة القراءة وفهم للنصوص المختلفة |
| | | | 7.2.3 إظهار الاستجابة المناسبة في السياقات التواصلية المختلفة |
| | | | 7.2.4 تطوير كـفـاءة القراءة وفهم للنصوص المختلفة بشكل صحيح |
| | | 7.3 التواصل بفعالية في سياقات مختلفة | 7.3.1 إنشاء النصوص باللغة الفصيحة في سـيـاقات مـخـتـلـفـة |
| | | 7.4 التفسيروالتحرير والترجمة للمعلومات السهلة | 7.4.1 تقديم التفسير السهل الصـحـيـح |
| | | | 7.4.2 القدرة على تحرير النصوص السهلة |
| | | | 7.4.3 إجراء الترجمة السهلة بصورة صحيحة |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| 8 | Kichina | 8.1 Kumudu stadi za msingi za lugha ya Kichina | 8.1.1 Kukuza ufahamu wa fonimu na matamshi ya awali, mwisho, toni na hanzi<br>8.1.2 Kumudu msamiati sahihi wa Kichina katika miktadha mbalimbali<br>8.1.3 Kukuza matumizi ya sarufi na msamiati mwafaka katika mazungumzo na maandishi |
| | | 8.2 Kuonesha uelewa wa taarifa za mdomo na za maandishi | 8.2.1 Kukuza umahiri wa kusikiliza na kuelewa taarifa<br>8.2.2 Kukuza umahiri wa kusoma na kuelewa matini mbalimbali<br>8.2.3 Kuonesha mwitiko sahihi katika miktadha mbalimbali ya kimawasiliano<br>8.2.4 Kukuza umahiri wa kusoma kwa usahihi matini mbalimbali |
| | | 8.3 Kuwasiliana kwa ufanisi katika miktadha mbalimbali | 8.3.1 Kukuza uelewa wa sifa za lugha ya mazungumzo na ya maandishi<br>8.3.2 Kukuza umahiri wa kuwasiliana kwa mdomo<br>8.3.3 Kukuza umahiri wa kuwasiliana kwa usahihi kwa maandishi katika miktadha mbalimbali |
| | | 8.4 Kutafsiri na kukalimani taarifa sahili | 8.4.1 Kutoa tafsiri sahili na sahihi<br>8.4.2 Kufanya ukalimani sahili kwa usahihi |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| 9 | Kifaransa | 9.1 Kumudu stadi za msingi za lugha ya Kifaransa | 9.1.1 Kukuza ufahamu wa fonimu na matamshi ya Kifaransa<br>9.1.2 Kumudu msamiati sahihi wa Kifaransa<br>9.1.3 Kukuza matumizi ya sarufi na msamiati mwafaka katika mazungumzo na maandishi |
| | | 9.2 Kuonesha uelewa wa taarifa zilizowasilishwa kwa mdomo na kwa maandishi | 9.2.1 Kukuza umahiri wa kusikiliza na kuelewa taarifa<br>9.2.2 Kukuza umahiri wa kusoma na kuelewa<br>9.2.3 Kuonesha mwitiko sahihi katika miktadha mbalimbali ya kimawasiliano<br>9.2.4 Kukuza umahiri wa kusoma kwa usahihi |
| | | 9.3 Kuwasiliana kwa ufanisi katika miktadha mbalimbali | 9.3.1 Kumudu sifa za lugha ya mazungumzo na ya maandishi<br>9.3.2 Kukuza umahiri wa kuwasiliana kwa mdomo<br>9.3.3 Kukuza umahiri wa kuwasiliana kwa maandishi |
| | | 9.4 Kutafsiri, kuhariri na kukalimani taarifa sahili | 9.4.1 Kutoa tafsiri sahili<br>9.4.2 Kufanya ukalimani<br>9.4.3 Kumudu uhariri wa matini sahili |
| 10 | Michezo | 10.1 Kuonesha uelewa wa dhana, usalama na maadili katika michezo | 10.1.1 Kutambua thamani ya michezo katika maisha ya mwanadamu<br>10.1.2 Kuzingatia miiko na maadili ya Kitanzania katika michezo |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | 10.2 Kuonesha uelewa wa umuhimu wa utimamu wa mwili na akili katika michezo | 10.2.1 Kutambua vijenzi vya utimamu wa mwili na akili katika michezo |
| | | 10.3 Kucheza michezo mbalimbali | 10.3.1 Kufanya mazoezi ya viungo<br>10.3.2 Kujenga stadi za michezo mbalimbali |
| | | 10.4 Kumudu misingi ya afya na usalama katika michezo | 10.4.1 Kutambua athari za tabia hatarishi katika michezo<br>10.4.2 Kuonesha uelewa wa uhusiano kati ya lishe na afya kwa wanamichezo |
| 11. | Baiolojia | 11.1 Kumudu dhana, misingi na michakato ya kibaiolojia | 11.1.1 Kufafanua michakato ya fiziolojia, anatomia na ikolojia kwa viumbe hai |
| | | 11.2 Kuwasiliana kwa kutumia majina na istilahi za kibaiolojia | 11.2.1 Kumudu istilahi za kibaiolojia |
| | | 11.3 Kufanya uchunguzi wa kibaiolojia | 11.3.1 Kumudu stadi za msingi za kufanya uchunguzi wa kibailojia<br>11.3.2 Kuandaa na kuwasilisha taarifa za uchunguzi wa kibailojia<br>11.3.3 Kufanya kazimradi kwa kutumia misingi ya kibaiolojia |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| 12 | Kemia | 12.1 Kumudu dhana, nadharia na kanuni za kikemia | 12.1.1 Kumudu dhana, nadharia na kanuni za kikemia<br>12.1.2 Kuainisha mabadiliko ya tabia ya kiumbo na kikemia ya vitu kwa kutumia mpangilio wa elementi katika jedwali |
| | | 12.2 Kuwasiliana kwa kutumia dhana za kikemia | 12.2.1 Kutumia kanuni za kimataifa kutaja majina sahihi ya vitu vya kikemia (IUPAC system)<br>12.2.2 Kutumia alama, fomula na milinganyo kuwasilisha matokeo ya mimenyuko |
| | | 12.3 Kufanya uchunguzi kwa kutumia misingi ya kikemia | 12.3.1 Kufanya majaribio ya kikemia |
| | | 12.4 Kumudu misingi ya uchenjuaji wa metali | 12.3.2 Kutumia kemikali na ujuzi wa teknolojia katika uchenjuaji wa metali |
| | | 12.5 Kufanya kazimradi ya kikemia | 12.5.1 Kufanya kazimradi kwa kutumia misingi ya kikemia |
| 13 | Fizikia | 13.1 Kutumia maarifa ya kifizikia katika miktadha mbalimbali | 13.1.1 Kumudu dhana, nadharia na kanuni za kifizikia<br>13.1.2 Kumudu misamiati, istilahi, vipimo na alama za kifizikia<br>13.1.3 Kutumia hisabati kuelezea kanuni na matukio ya kifizikia |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | 13.2 Kufanya uchunguzi wa kifizikia | 13.2.1 Kumudu stadi za msingi kufanya uchunguzi wa kifizikia<br>13.2.2 Kuchambua taarifa za uchunguzi wa kifizikia na kuwasilisha matokeo |
| | | 13.3 Kutathmini na kutumia taarifa za kifizikia | 13.3.1 Kukusanya, kuelezea na kuhusianisha data za kifizikia<br>13.3.2 Kufanya kazimradi za kifizikia |
| 14 | Kilimo | 14.1 Kumudu kanuni za kilimo bora | 14.1.1 Kuelewa kanuni na misingi ya kilimo bora |
| | | 14.2 Kutumia stadi za kilimo bora | 14.2.1 Kutumia kanuni na mbinu za msingi za kilimo kwa uzalishaji wenye tija wa mazao mkakati<br>14.2.2 Kutumia kanuni za msingi za ufugaji kuongeza tija<br>14.2.3 Kutumia kanuni za msingi za uzalishaji wa viumbe maji |
| | | 14.4 Kufanya uchunguzi na majaribio ya kisayansi katika uzalishaji wa mazao ya kilimo | 14.4.1 Kuandaa na kuwasilisha taarifa za uchunguzi |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| 15 | Hisabati | 15.1 Kumudu lugha ya kihisabati | 15.1.1 Kutumia stadi za namba katika mazingira tofauti<br>15.1.2 Kutumia stadi za uwiano, faida na hasara katika maisha ya kila siku<br>15.1.3 Kutumia stadi za kupungua na kuongezeka katika miktadha mbalimbali |
| | | 15.2 Kufikiri kimantiki katika kutafsiri na kutatua changamoto mbalimbali | 15.2.1 Kutumia stadi za kijometri, kukadiria, uhusiano na functions kufanya maamuzi katika miktadha mbalimbali<br>15.2.2 Kutumia stadi za aljebra na matrices katika kutatua matatizo<br>15.2.3 Kutumia stadi za seti, mpangilio na mtiririko wa namba katika kutatua matatizo |
| | | 15.3 Kumudu dhana za msingi katika majira ya nukta, trigonometry, vector, yumkini (probability) na takwimu | 15.3.1 Kutumia stadi za msingi za majira ya nukta, trigonometry na vector katika maisha ya kila siku<br>15.3.2 Kutumia stadi za kutabiri (probability) katika maisha ya kila siku<br>15.3.3 Kutumia stadi za takwimu katika maisha ya kila siku |
| 16 | Additional Mathematics | 16.1 Kutumia maarifa na stadi za juu za kihisabati katika maisha ya kila siku | 16.1.1 Kutumia stadi za juu za majira ya nukta, trigonometric, vectors na geometrical construction katika maisha ya kila siku |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | | 16.1.2 Kutumia stadi za takwimu katika fani za biashara na uchumi<br>16.1.3 Kumudu stadi za kimantiki katika kufanya maamuzi<br>16.1.4 Kutumia stadi za kutabiri katika maisha ya kila siku |
| | | 16.2 Kumudu misingi ya Algebra na calculus katika kutatua matatizo mbalimbali | 16.2.1 Kutumia Algebra na calculus kutatua matatizo mbalimbali<br>16.2.2 Kutumia stadi za seti katika kufanya maamuzi |
| 17. | Computer Science | 17.1 Demonstrate mastery of the basic Concepts of Computer Science | 17.1.1 Demonstrate an understanding the field of Computer Science and its related fields<br>17.1.2 Demonstrate an understanding of computer systems<br>17.1.3 Demonstrate mastery of maintenance and troubleshooting of computer systems<br>17.1.4 Demonstrate mastery of basics of system administration<br>17.1.5 Demonstrate mastery of the Internet, and basics of cyber security |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
| --- | --- | --- | --- |
| | | 17.2 Demonstrate mastery of the basic principles of Computer Science | 17.2.1 Demonstrate mastery of the basic principles of problem solving (concept of problem solving, steps of problem solving, concept of algorithms)<br>17.2.2 Demonstrate an understanding of basic principles of computer programming (using an appropriate structured programming language such as C, python, etc)<br>17.2.3 Demonstrate an understanding of the basic principles of computer architecture.<br>17.2.4 Demonstrate an understanding of the basics of computer networks<br>17.2.5 Demonstrate mastery of basic principles of web develop- ment (HTML, CSS, and Ja- vaScript)<br>17.2.6 Demonstrate mastery of basic principles of mobile App |
| | | 17.3 Demonstrate mastery of the basic principles of data management | 17.3.1 Demonstrate the mastery of basic principles of databas- es and database management systems. |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | | 17.3.2 Demonstrate the mastery of the basic principles of data analysis (data collection, pre-processing, processing, visualization, interpretation) |
| 18 | Utunzaji wa Taarifa za Fedha | 18.1 Kumudu misingi ya utunzaji wa taarifa za fedha | 18.1.1 Kuonesha uelewa wa misingi na nadharia za utunzaji wa taarifa za fedha<br>18.1.2 Kurekodi miamala ya biashara kwa kutumia hati chanzo<br>18.1.3 Kuandaa urari kukagua usahihi wa hesabu za fedha |
| | | 18.2 Kutengeneza taarifa za msingi za fedha kwa ajili ya ukaguzi | 18.2.1 Kuandaa taarifa za msingi za faida au hasara ya biashara<br>18.2.2 Kuandaa taarifa za msingi za hali ya kifedha ya biashara<br>18.2.3 Kuandaa taarifa ya mtiririko wa fedha<br>18.2.4 Kuandaa taarifa za msingi za fedha wa ajili ya ukaguzi |
| | | 18.3 Kutumia taarifa za kifedha za taasisi zisizo za kibiashara | 18.3.1 Kuonesha uelewa wa tofauti kati ya mashirika ya kibiashara na mashirika yasiyo ya kibiashara<br>18.3.2 Kutengeneza taarifa za kifedha za mashirika yasiyo ya kibiashara |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | 18.4 Kumudu taratibu za udhibiti wa fedha | 18.4.1 Kufanya ulinganisho wa taarifa za fedha baina ya benki na taasisi (Bank Reconciliation Statement)<br>18.4.2 Kuandaa bajeti<br>18.4.3 Kurekodi miamala ya fedha kwa kutumia mifumo mbalimbali na kurekebisha makosa katika vitabu vya fedha |
| | | 18.5 Kumudu matumizi ya TEHAMA katika utunzaji wa fedha | 18.5.1 Kutumia programu sahili za kompyuta katika utunzaji wa fedha (basic accounting packages) |
| 19 | Elimu ya Biashara | 19.1 Kumudu maarifa ya kibiashara | 19.1.1 Kumudu dhana, nadharia, na kanuni za Elimu ya Biashara |
| | | 19.2 Kutatua changamoto za kijamii kwa kutumia stadi za kibiashara | 19.2.1 Kumudu kuendesha na kusimamia biashara ndogondogo<br>19.2.2 Kumudu kununua na kuuza bidhaa ndani na nje ya nchi |
| | | 19.3 Kutumia maarifa ya kibiashara katika miktadha mbalimbali | 19.3.1 Kutafsiri nadharia za kibiashara kwa vitendo<br>19.3.2 Kuonesha uelewa wa awali wa maadili ya biashara |
| 20 | Ushoni | 20.1 Demonstrate mastery of basic concepts and principles of garment construction | 201.1 Demonstrate an understanding of basic principles of garment construction<br>20.1.2 Caring for clothes and house hold articles |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | 20.2 Demonstrate mastery of garment construction | 20.2.1 Demonstrate an understanding of the concept of patterns in garment construction<br>20.2.2 Select the right fabric for different garments (design, style, fashion, texture, colour and line in garment construction)<br>20.2.3 Sew simple styles of various garments (lay and cut out, apply procedures of garment construction) |
| | | 20.3 Demonstrate mastery of professionalism and ethics in garment construction | 20.3.1 Demonstrate an understanding in operating a textile related business<br>20.3.2 Demonstrate an understanding of professionalism and ethics in tailoring |
| 21 | Sanaa Sanifu | 21.1 Kumudu, dhana, nadharia, misingi na kanuni za sanaa sanifu | 21.1.1 Kuonesha uelewa wa dhana, nadharia, misingi na kanuni za sanaa sanifu<br>21.1.2 Kuonesha uelewa wa matapo ya sanaa sanifu Tanzania |
| | | 21.2 Kutengeneza kazi sahili za sanaa sanifu | 21.2.1 Kutengeneza vitu kwa ajili ya matumizi na mapambo<br>21.2.2 Kutumia mbinu za asili na za kisasa kutengeneza kazi za sanaa<br>21.2.3 Kutengeneza maudhui halisi ya sanaa |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
| --- | --- | --- | --- |
| | | 21.3 Kuzingatia kanuni za usalama kazini, mazingira na afya katika shughuli za sanaa sanifu | 21.3.1 Kuteketeza au kuhifadhi aina tofauti za taka katika shughuli za sanaa sanifu<br>21.3.2 Kuonesha uelewa wa maadili katika tasnia ya sanaa sanifu |
| | | 21.4 Kutumia TEHAMA kutangaza kazi za sanaa sanifu | 21.4.1 Kutumia TEHAMA kutangaza kazi za sanaa sanifu |
| 22. | Muziki | 22.1 Kumudu dhana, nadharia, misingi na kanuni za muziki | 22.1.1 Kuonesha uelewa wa dhana, nadharia, misingi na kanuni za muziki<br>22.1.2 Kuonesha uelewa wa kanuni za msingi za kusoma na kuandika muziki |
| | | 22.2 Kumudu kazi za muziki | 22.2.1 Kuimba nyimbo za kitamaduni na za kigeni<br>22.2.2 Kupiga ala za muziki za asili na za kigeni<br>22.2.3 Kumudu misingi ya maadili katika tasnia ya muziki |
| | | 22.3 Kumudu matumizi ya TEHAMA katika shughuli za muziki | 22.3.1 Kutumia programu za kompyuta kuandika muziki<br>22.3.2 Kutumia TEHAMA katika uzalishaji wa muziki |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | | 22.3.3 Kutumia TEHAMA kuhifadhi kazi za muziki<br>22.3.4 Kutumia TEHAMA kutafuta soko na kutangaza kazi za muziki |
| | | 22.4 Kufanya utafiti wa muziki | 24.4.1 Kufanya utafiti mdogo wa soko la muziki |
| 23 | Sanaa za Maonyesho | 23.1 Kumudu dhana, nadharia, misingi na kanuni za sanaa za maonyesho | 23.1.1 Kumudu uelewa wa dhana na historia ya sanaa za maonyesho<br>23.1.2 Kuonesha uelewa wa nadharia na kanuni za sanaa za maonyesho<br>23.1.3 Kuonesha uelewa wa mchango wa sanaa za maonyesho katika maendeleo ya jamii |
| | | 23.2 Kumudu sanaa za maonyesho | 23.2.1 Kufanya sanaa za maonyesho kwa kuzingatia aina za hadhira<br>23.2.2 Kutumia TEHAMA kuandaa maigizo sahili ya televisheni, filamu na redio<br>23.2.3 Kutumia sanaa kwa maendeleo kutatua matatizo ya jamii<br>23.2.4 Kumudu misingi ya maadili katika uandaaji na uwasilishaji wa kazi za sanaa za maonyesho |
| | | 23.3 Kumudu matumizi ya lugha bunifu katika sanaa za maonyesho | 23.3.1 Kutumia lugha ya kibunifu katika kuandaa kazi za sanaa za maonyesho |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | | 23.3.2 Kutafsiri sanaa za maonyesho katika miktadha mbalimbali kwa kuzingatia hadhira husika |
| | | 23.4 Kumudu misingi ya biashara ya sanaa za maonyesho | 23.4.1 Kubuni mawazo na fursa za biashara kupitia sanaa za maonyesho<br>23.4.2 Kuchambua gharama za utengenezaji na uuzaji wa kazi za sanaa za maonyesho<br>23.4.3 Kubuni mikakati ya kutafuta soko la kazi za sanaa za maonyesho |
| 24 | Chakula na Lishe | 24.1 Demonstrate mastery of the basic principles of Food and Nutrition | 24.1.1 Describe the basic principles of Food and Nutrition<br>24.1.2 Describe the nutrient content of different foods<br>24.1.3 Demonstrate mastery of the principles of cookery |
| | | 24.2 Demonstrate an understanding of the relationship between health and nutrition | 24.2.1 Describe the relationship between health and nutrition<br>24.2.2 Use of food and nutrition principles to improve health |
| | | 24.3 Demonstrate mastery of cookery | 24.3.1 Prepare a balanced meal based on different foods available in the community |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | | 24.3.2 Prepare a balanced meal for people with different nutritional needs<br>24.3.3 Demonstrate mastery of cooking for business purposes |
| | | 24.4 Demonstrate mastery of using technology to preserve food | 24.4.1 Design and use simple technology to preserve different types of foodi |
| | | 24.5 Carry out a project in food and Nutrition | 24.5.1 Conduct a project in food and Nutrition |
| 25 | Elimu ya Dini ya Kikristo | 25.1 Kuheshimu uumbaji na amri za Mungu | 25.1.1 Kutumia Kitabu cha Mwanzo kujifunza uumbaji, uwajibikaji na kutunza uhai<br>25.1.2 Kumudu Maandiko Matakatifu kwa kutumia Kitabu cha Mwanzo<br>25.1.3 Kutumia Kitabu cha Kutoka kujifunza upendo na huruma ya Mungu<br>25.1.4 Kutathmini amri za Mungu kama zilivyobainishwa katika Kitabu cha Kutoka<br>25.1.5 Kutathmini umuhimu wa takwimu kwa kutumia Kitabu cha Hesabu |
| | | 25.2 Kuonesha uelewa wa imani na kuishi kwa kumtii Mungu | 25.2.1 Kumudu Maandiko Matakatifu katika Kitabu cha Joshua |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | | 25.2.2 Kutumia Kitabu cha Joshua kujifunza uhodari, ushujaa, unyenyekevu, ustahimilivu na uzalendo |
| | | 25.3 Kutumia Biblia kumjua, kumpenda na kumtumikia Mungu | 25.3.1 Kumudu Maandiko Matakatifu katika Injili kama ilivyoandikwa na Luka<br>25.3.2 Kutumia Injili kama ilivyoandikwa na Luka kujifunza malezi na maisha bora ya familia<br>25.3.3 Kumudu Maandiko Matakatifu katika Kitabu cha Matendo ya Mitume<br>25.3.4 Kuonesha uelewa wa umuhimu wa kumtumikia Mungu katika kueneza Injili<br>25.3.5 Kuonesha uelewa wa umuhimu wa haki, amani na usawa kwa mujibu wa Kitabu cha Matendo ya Mitume |
| 26 | Elimu ya Dini ya Kiislamu | 26.1 Kuonesha uelewa wa aina za Tawhidi na Daraja za dini (Maratibu Diin) | 26.1.1 Kuchambua aina za Tawhid na Daraja za dini katika maisha ya Muislamu<br>26.1.2 Kufafanua misingi ya Dini ya Kiislamu<br>26.1.3 Kutumia mwenendo/Sira za Mtume Muhammad (S.A.W) |
| | | 26.2 Kutumia Qur'an na Sunnah katika maisha ya kila siku | 26.2.1 Kusoma kwa hifdhi na ahkam Sura thelathini (30) kutoka mwisho wa Qur'an Tukufu<br>26.2.2 Kuchambua mafunzo ya Aya zilizochaguliwa |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | | 26.2.3 Kuchanganua mafunzo ya Hadithi zilizochaguliwa |
| | | 26.3 Kufanya ibada za Faradhi na Sunnah kwa usahihi | 26.3.1 Kuchambua utekelezaji wa nguzo tano za Uislamu na umuhimu wake<br>26.3.2 Kuchanganua miamala halali na haramu katika Uisilamu |
| | | 26.4 Kutekeleza matendo mema, kufanya kazi za kiuchumi na kutumia mali kwa usahihi | 26.4.1 Kuchambua maadili na tabia kutokana na kazi za uchumi na biashara za Mtume Muhammad (S.A.W)<br>26.4.2 Kuchambua maadili na tabia za Mtume Muhammad (S.A.W) katika miamala ya ajira<br>26.4.3 Kuchambua maadili na tabia za Mtume Muhammad (S.A.W) katika kazi za uongozi/ukhalifa |
| | | 26.5 Kuishi kwa kumuiga Mtume Muhammad (S.A.W) na Makhalifa waongofu katika maisha ya kila siku | 26.5.1 Kuchambua imani, mila na amali za washirikina kabla, wakati na baada ya Mtume Muhammad (S.A.W)<br>26.5.2 Kuchambua mafunzo ya Sira ya Mtume Muhammad (S.A.W) na Makhalifa wake |
| | | 26.6 Kuamrisha mema na kukataza maovu katika jamii | 26.6.1 Kutumia Aya na Hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W) zilizoteuliwa |

| Na. | Somo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| 27 | Fasihi ya Kiswahili | 27.1 Kuthamini kazi za fasihi ya Kiswahili | 27.1.1 Kuonesha uelewa wa kazi za fasihi ya Kiswahili ya kitaifa<br>27.1.2 Kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili |
| | | 27.2 Kujenga ujumi kutokana na kazi za fasihi | 27.2.1 Kujenga ujumi na falsafa ya Kiafrika katika kazi za fasihi<br>27.2.2 Kutumia kazi za fasihi katika kujenga hoja zenye mantiki |
| | | 27.3 Kubuni kazi za fasihi | 27.3.1 Kutathmini mbinu za kisanaa za utunzi wa kazi za kifasihi<br>27.3.2 Kutunga kazi sahili za kifasihi 27.3.3 Kutambua fursa zinazotokana na fasihi ya Kiswahili |

## Sehemu ya Nne

## Ufundishaji na Ujifunzaji

Mtaala huu unasisitiza matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji na mwalimu kuwa mwezeshaji. Mwalimu atatumia mbinu zinazomshirikisha mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia somo, mahitaji anuai na uwezo wa mwanafunzi. Mbinu zitakazotumika ni pamoja na matumizi ya michezo na sanaa, TEHAMA na teknolojia zingine saidizi, majaribio ya kisayansi, ziara za kimasomo, majadiliano, matembezi darasani na mbinu zingine shirikishi zinazohamasisha ujifunzaji. Aidha, Mtaala unasisitiza mwalimu kuwa mbunifu na mnyumbufu katika kutumia zana halisi zinazopatikana katika mazingira yake na kutengeneza mazingira ya mwanafunzi kutumia zana hizo katika ujifunzaji.

### 4.1 Masuala Mtambuka

Masuala mtambuka ni miongoni mwa mambo muhimu yaliyozingatiwa katika mtaala huu. Wanafunzi watajifunza masuala mtambuka kama vile mazingira, afya, elimu jumuishi, elimu ya jinsia, elimu ya amani, maadili, haki na wajibu wa mtoto, haki za binadamu, ulinzi na usalama, usalama barabarani, elimu ya fedha, elimu ya rushwa, ushirika na masuala ya muungano. Masuala haya yatachopekwa kwenye masomo bebezi wakati wa vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uhusiano wa suala mtambuka na somo husika.

### 4.2 Muda na Idadi ya Vipindi

Mwaka wa masomo utakuwa na siku 194 sawa na wiki 39 ambazo zimegawanyika katika mihula miwili inayolingana. Katika kila muhula wiki mbili zitatumika kwa upimaji wa ndani. Muda wa kipindi utakuwa dakika 40 na muda wa kusoma kwa siku ni saa 6. Mgawanyiko wa vipindi na muda kwa kila somo katika kila ngazi ya Elimu ya Sekondari umefafanuliwa katika Jedwali Na. 5. hadi 6.

**Jedwali Na. 5:** *Masomo ya Msingi na Lazima na Idadi ya Vipindi kwa Wiki*

| Na | Masomo | Idadi ya Vipindi kwa Wiki | |
|---|---|---|---|
| | | Kidato cha I - II | Kidato cha III - IV |
| 1. | Mathematics | 5 | 5 |
| 2. | Kiswahili | 4 | 4 |
| 3. | English Language | 5 | 5 |
| 4. | Business Studies | 3 | 3 |
| 5. | Geography | 2 | 3 |
| 6. | Historia ya Tanzania na Maadili | 3 | 3 |

**Jedwali Na. 6:** *Masomo Chaguzi na Idadi ya Vipindi kwa Wiki*

| Na | Somo | Idadi ya Vipindi kwa Wiki | |
|---|---|---|---|
| | | Kidato cha I - II | Kidato cha III - IV |
| 1. | Physics | 3 | 4 |
| 2. | Chemistry | 3 | 4 |
| 3. | Biology | 3 | 4 |
| 4. | Agriculture | 5 | 5 |
| 5. | Computer science | 4 | 4 |
| 6. | Food and Human Nutrition | 5 | 5 |
| 7. | Sport Studies | 4 | 4 |
| 8 | Textile and Garment Construction | 5 | 5 |
| 9. | Fine Art | 4 | 4 |
| 10. | Theatre Arts | 4 | 4 |
| 11. | Additional Mathematics | - | 3 |
| 12. | Literature in English | - | 2 |
| 13. | Fasihi ya Kiswahili | - | 2 |

| Na | Somo | Idadi ya Vipindi kwa Wiki | |
|---|---|---|---|
| | | Kidato cha I - II | Kidato cha III - IV |
| 14. | French | 3 | 3 |
| 15. | Arabic | 3 | 3 |
| 16. | Chinese | 3 | 3 |
| 17. | Music | 4 | 4 |
| 18. | History | 3 | 4 |
| 19. | Book-keeping | 3 | 4 |
| 20. | Bible Knowledge | 3 | 3 |
| 21. | Dini ya Kiislamu | 3 | 3 |

Muda uliotengwa kwa mkondo wa elimu ya amali ni saa 1500 kwa mwaka. Mchanganuo wa muda umeanishwa kwenye Jedwali Na. 7. Mgawanyo wa saa kwa masomo ya elimu ya amali utazingatia Mtaala wa fani husika ulioidhinishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET). Aidha, shughuli za ziada nje ya mtaala zitatekelezwa kwa kufuata miongozo inayotolewa na mamlaka husika.

**Jedwali Na 7:** *Mgawanyo wa Muda kwa Mkondo wa Elimu ya Amali*

| Na. | Mchanganuo | Muda (saa kwa mwaka) | |
|---|---|---|---|
| | | Kidato cha I& II | Kidato cha III& IV |
| 1. | Masomo ya Amali | 870 | 720 |
| 2. | Masomo za Taaluma | 480 | 480 |
| 3. | Kazimradi | - | 150 |
| 4. | Mitihani | 150 | 150 |
| | **Jumla** | **1500** | **1500** |

### 4.3 Lugha ya Kufundishia na Kujifunzia

*Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014* Toleo la Mwaka 2023 inaelekeza matumizi ya lugha ya Kiswahili, Kiingereza pamoja na lugha nyingine za kigeni katika elimu na mafunzo. Aidha, Sera inatamka kuwa lugha ya kufundishia na kujifunzia katika elimu ya sekondari ni Kiingereza. Masomo ya Kiswahili, *English Language*, Kifaransa, Kichina na Kiarabu yatafundishwa kwa lugha husika.

## Sehemu ya Tano

## Upimaji na Tathmini ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Upimaji katika elimu hufanyika kwa lengo la kubaini maendeleo ya mwanafunzi kwa kile anachokijua, anachoweza kufanya, mabadiliko ya tabia na mwelekeo na kubaini changamoto ya mwanafunzi katika kujifunza ili kuzitafutia ufumbuzi kwa wakati. Aidha, upimaji ukitumika vizuri huamsha ari ya mwanafunzi kujifunza zaidi na kuboresha ufundishaji. Kama ilivyobainishwa katika *Sera ya Elimu na Mafunzo* ya Mwaka 2014 Toleo la Mwaka 2023, mtaala huu unalenga kuimarisha upimaji na tathmini ya maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma. Mtaala huu utatumia mfumo wa upimaji endelevu, upimaji wezeshi na upimaji tamati kwa kuzingatia vigezo vya upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi vinavyotambulikaili kujenga umahiri katika ujifunzaji. . Upimaji wa ndani utaratibiwa shuleni sambamba na ufundishaji na ujifunzaji na upimaji wa nje utaratibiwa na kutekelezwa na mamlaka husika zikiwemo Baraza la Mitihani la Tanzania na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ili kuhakikisha uthabiti na kuaminika kwa upimaji wa ndani.

### 5.1 Upimaji wa Masomo ya Taaluma

#### 5.1.1 Upimaji Wezeshi

Upimaji wezeshi ni upimaji unaofanyika wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ili kusaidia au kuwezesha ujifunzaji fanisi kwa mwanafunzi. Lengo la upimaji huu ni kusaidia mwanafunzi na mwalimu kubaini maeneo ambayo mwanafunzi ameyaelewa na maeneo ambayo ana changamoto na hivyo kumwezesha kutafuta suluhu ya changamoto inayomkabili kwa wakati. Upimaji wezeshi unaweza kufanyika kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwamo kuuliza maswali, kutoa mrejesho, mwanafunzi kubaini lengo au malengo ya ujifunzaji, mwanafunzi kujipima mwenyewe au kupimwa na wanafunzi wenzake na kutumia matokeo ya upimaji tamati kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Matumizi ya mbinu hizi yatamwezesha mwalimu kubaini uelewa na changamoto zinazowakabili wanafunzi wakati mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unaendelea na hivyo kwa pamoja kuweka mikakati ya utatuzi.

### 5.1.2 Upimaji Endelevu

Upimaji endelevu hufanyika wakati wote wa ufundishaji na ujifunzaji ndani na nje ya darasa. Upimaji huu humsaidia mwalimu kubaini ufanisi katika utendaji wa shughuli mbalimbali za kila siku za mwanafunzi. Pia, upimaji huu humwezesha mwalimu na mwanafunzi kujua ni eneo gani amefanikiwa au hajafanikiwa ili kuweka mkakati wa kuboresha na kuimarisha ujifunzaji. Vilevile, upimaji huu utamwezesha mwalimu kubaini vipaji mbalimbali vya mwanafunzi kama vile ubunifu, uchoraji, sanaa na michezo. Upimaji endelevu utachangia asilimia 30 ya upimaji wa mwisho wa Kidato cha IV. Mchanganuo wa alama za upimaji endelevu kwa masomo yaliyoanza kufundishwa Elimu ya Msingi Darasa la III kwa mfano Historia ya Tanzania na Maadili, Hisabati, *English Language,* Kichina, Kifaransa, Kiarabu na Kiswahili, alama zake za Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la VI zitachangia katika upimaji endelevu Kidato cha IV kama ilivyo kwenye Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na. 8:** *Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu na Tamati kwa Masomo Yaliyoanza Kufundishwa Darasa la III*

| Na. | Aina ya upimaji | Asilimia |
|---|---|---|
| 1. | Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la VI | 5.0 |
| 2. | Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha II | 6.0 |
| 3. | Mtihani wa Muhula wa Pili wa Kidato cha III | 5.0 |
| 4. | Kazimradi | 7.0 |
| 5. | Mtihani wa Utamilifu wa Kidato cha IV | 7.0 |
| 6. | Mtihani wa Taifa wa Kidato cha IV | 70.0 |
| **Jumla** | | **100.0** |

Aidha, kwa masomo yanayoanza kufundishwa Kidato cha I, mchanganuo wa alama za upimaji endelevu ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na. 9.

**Jedwali Na. 9:** *Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu na Tamati kwa Masomo Yanayoanza Kufundishwa Kidato cha I*

| Na. | Aina ya upimaji | Asilimia |
|---|---|---|
| 1. | Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha II | 6.0 |
| 2. | Mtihani wa Muhula wa Kwanza wa Kidato cha III | 5.0 |
| 3. | Mtihani wa Muhula wa Pili wa Kidato cha III | 5.0 |
| 4. | Kazimradi | 7.0 |
| 5. | Mtihani wa Utamilifu wa Kidato cha IV | 7.0 |
| 6. | Mtihani wa Taifa wa Kidato cha IV | 70.0 |
| **Jumla** | | **100.0** |

Masomo yanayoanza kufundishwa Kidato cha III, mchanganuo wa alama za upimaji endelevu ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na. 10.

**Jedwali Na.10:** *Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu na Tamati kwa Masomo Yanayoanza Kufundishwa Kidato cha III*

| Na. | Aina ya upimaji | % |
|---|---|---|
| 1. | Mtihani wa Muhula wa Kwanza wa Kidato cha III | 5.0 |
| 2. | Mtihani wa Muhula wa Pili wa Kidato cha III | 5.0 |
| 3. | Mtihani wa Muhula wa Kwanza wa Kidato cha IV | 6.0 |
| 4. | Kazimradi | 7.0 |
| 5. | Mtihani wa Utamilifu wa Kidato cha IV | 7.0 |
| 6. | Mtihani wa Taifa wa Kidato cha IV | 70.0 |
| **Jumla** | | **100.0** |

### 5.1.3 Upimaji Tamati

Upimaji tamati utafanyika mwishoni mwa kila muhula. Aidha, upimaji tamati unahusisha upimaji wa kitaifa utakaofanyika mwishoni mwa Kidato cha II na upimaji wa mwisho wa Kidato cha IV. Upimaji wa Kidato cha II lengo lake ni kubaini kama mwanafunzi amefikia umahiri unaotarajiwa ili aweze kuendelea na Kidato cha III. Matokeo ya upimaji huu yatatumika kama sehemu ya upimaji endelevu katika mtihani wa mwisho wa Kidato cha IV. Upimaji wa mwisho wa Kidato cha IV unalenga kupata taarifa na uelewa wa kiwango cha umahiri ambacho mwanafunzi amefikia. Pia, upimaji huu utasaidia kubaini ni kwa kiasi gani malengo katika ngazi ya Elimu ya Sekondari

Kidato cha I - IV yamefikiwa. Ili mwanafunzi ahitimu ngazi hii, anatakiwa afanye mtihani wa taifa mwishoni mwa Kidato cha IV. Baraza la Mitihani la Tanzania litahusika na upimaji huu. Mhitimu wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV atapata cheti kuonesha kuwa amehitimu hatua hii. Upimaji huu utachangia asilimia 70 ya upimaji wote.

#### 5.1.4 Zana na Mbinu za Upimaji na Tathmini

Zana na mbinu mbalimbali za upimaji zitatumika kupima nadharia na vitendo katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji. Mbinu zitakazotumika ni pamoja na uchunguzi, majaribio, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi) na kazimradi. Mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mitihani ya mwisho. Aidha, mtaala unasisitiza kutumia zana za upimaji na tathmini kama vile orodha hakiki, dodoso na mkoba wa kazi. Matumizi ya mbinu na zana hizi yatatofautiana kulingana na sababu ya upimaji, aina na mahitaji ya somo, mahitaji anuai ya mwanafunzi na umahiri unaokusudiwa kujengwa.

### 5.2 Upimaji wa Fani za Elimu ya Amali

Upimaji wa fani za elimu ya amali utafanyika kwa kuzingatia miongozo ya mitihani, taratibu na miongozo ya utahini na utunuku ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Wanafunzi wote wa Mkondo wa Elimu ya Amali watafanya mitihani ya NACTVET wakiwa Kidato cha II (NVA ngazi ya 1), Kidato cha III (NVA ngazi ya 2) na Kidato cha IV (NVA ngazi ya 3).

NACTVET itatunuku cheti cha umahiri baada ya mwanafunzi kufuzu wa ngazi husika.

## Sehemu ya Sita

## Rasilimali za Utekelezaji wa Mtaala

Rasilimali za utekelezaji wa mtaala zinahusisha rasilimali watu, vitu, muda na fedha. Viwango na sifa stahiki za rasilimali hizi zinatolewa na wizara yenye dhamana kupitia miongozo mbalimbali. Aidha, baadhi ya rasilimali hizo ni watu, vitu, samani na majengo, muda na fedha.

### 6.1 Rasilimali Watu

Rasilimali watu inayohitajika katika utekelezaji wa mtaala inajumuisha walimu mahiri na watumishi mwega (watumishi waendeshaji wasiokuwa walimu). Aidha, mwalimu atakayefundisha Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV Elimu ya Jumla anatakiwa awe angalau na Shahada ya Ualimu kwa masomo atakayofundisha katoka chuo kinachotambulika na Serikali. Mwalimu mahiri katika Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV Elimu ya Amali anatakiwa awe amehitimu Stashahada au Shahada ya fani husika na kupata mafunzo ya ualimu kwa muda usiopungua mwaka mmoja. Mwalimu anatakiwa aweze kufundisha, kupima na kufanya tathmini. Sifa zaidi za mwalimu zimefafanuliwa kwenye Kiunzi cha Umahiri wa Mwalimu kilichoandaliwa na wizara inayohusika na elimu.

Watumishi mwega ni kiungo muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa mtaala huu. Kundi hili linajumuisha wataalamu kama vile wakutubi, wataalamu wa maabara, wataalamu wa karakana, wauguzi, makatibu muhtasi, wasidizi wa ofisi, walinzi na wengine. Wafanyakazi hawa watapaswa kuwa wamepata mafunzo katika chuo kinachotambulika na serikali na wamefuzu katika fani husika

### 6.2 Rasilimali Vitu

Rasilimali vitu inahusisha vifaa mbalimbali vitakavyosaidia utekelezaji wa mtaala. Rasilimali hizo ni pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ambavyo vinajumuisha mihtasari, miongozo, vitabu vya kiada na ziada na zana za kufundishia na kujifunzia. Vifaa vingine ni vifaa vya sayansi na TEHAMA kama vile vifani, vinasa sauti na kompyuta. Rasilimali vitu inajumuisha viwanja vya michezo, vifaa vya michezo, sanaa na fani mbalimbali. Aidha, vifaa vingine muhimu kwa utekelezaji wa mtaala ni vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Vifaa hivi ni vile vya kusaidia kuona, kusikia na kugusa kama vile mashine za Breli, vitabu vya sauti, vikuza sauti na vikuza

maandishi kwa wenye uoni hafifu. Ili kuthibiti ubora, vifaa vitakavyotumika shuleni ni vile vilivyothibitishwa na Wizara inayohusika na elimu.

### 6.3 Samani na Majengo

Samani na majengo ni miongoni mwa rasilimali muhimu katika utekelezaji wa mtaala. Majengo yanajumuisha madarasa, maabara, karakana, maktaba, ofisi za walimu, mabweni, kumbi, jengo la kutolea huduma za afya na jiko. Samani na majengo hayo yazingatie wanafunzi wa aina zote wakiwemo wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Samani na majengo kwa utekelezaji wa elimu ya amali yanatakiwa kutoa nafasi kwa mwanafunzi kujifunza kwa vitendo. Hivyo, samani na majengo yatazingatia mwongozo uliowekwa na Wizara inayohusika na elimu.

### 6.4 Rasilimali Muda

Muda wa utekelezaji wa Mtaala huu ni miaka minne (4) yenye mihula miwili kwa kila mwaka wa masomo. Siku za masomo kwa mwaka ni 194 ambazo ni sawa na wiki 39 kama ilivyofafanuliwa kwenye Jedwali Na. 3. hadi 4. Kalenda ya masomo itatolewa na Wizara yenye dhamana ya kusimamia elimu. Hivyo, wazazi, walezi, jamii, serikali na wadau mbalimbali wa elimu wanatakiwa kuhakikisha kuwa muda uliopangwa unatumika vema katika kutekeleza mtaala huu.

### 6.5 Rasilimali Fedha

Utekelezaji wa mtaala utategemea uwepo wa rasilimali fedha za kutosha. Rasilimali hii itapatikana kupitia uchangiaji wa fedha na mali kutoka kwa wadau mbalimbali. Serikali ikishirikiana na sekta binafsi pamoja na wabia wa maendeleo ya elimu katika kuhakisha kuwa kunakuwepo na rasilimali fedha yakutosha ili kufanikisha utekelezaji wa mtaala huu.

### 6.6 Ushiriki wa Wadau katika Utekelezaji wa Mtaala

Ushirikishwaji wa wazazi au walezi na wadau wengine wa elimu ni muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa mtaala huu. Shule za sekondari zitashirikiana na wadau hawa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa katika utoaji wa Elimu ya Sekondari.

## 6.7 Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Mtaala

Usimamizi wa utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV utafanyika kuanzia ngazi ya shule hadi wizara kulingana na miongozo iliyowekwa na Wizara inayohusika na elimu. Usimamizi wa mtaala ngazi ya shule utafanywa na mkuu wa shule kwa kushirikiana na Bodi ya shule, Maafisa Elimu Wilaya, Mkoa na Wathibiti Ubora wa Shule. Kwa upande wa Elimu ya Amali, VETA pia itahusika katika ufuatiliaji na tathmini.

Aidha, ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV unalenga kupata mrejesho wa namna mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unavyofanyika ikihusisha mafanikio, changamoto na namna yakuzitatua ili kufikia malengo.

**Bibliografia**


Charter, A. (1990). *African charter on the rights and welfare of the child.* African Union.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (1982). *Mfumo wa Elimu Tanzania 1981-2000. Ripoti na maendeleo ya tume ya Rais ya Elimu*. Juzuu la Pili.

KICD. (2017). *Basic education curriculum framework.* Kenya Institute of Curriculum Development.

Lakkala, S., Uusiautti, S., & Määttä, K. (2016). How to make the neighbourhood school a school for all? Finnish teachers' perceptions of educational reform aiming towards inclusion. *Journal of Research in Special Educational Needs*, *16*(1), 46-56.

Mauritius Institute of Education. (2015). *National curriculum framework nine year continuous.* Mauritius Institute of Education.

Ministry of Education and Vocational Training. (2014). *Education and training policy.* MoEC.

Ministry of Education, Science and Technology. (2019). N*ational curriculum framework for basic and teacher education.* Tanzania Institute of Education.

Ministry of Education, Science and Technology. (2022). *National strategy for inclusive education in Tanzania* 2021/22 -2025/26. MoEST.

Ministry of Education and Vocational Training. (2009). *National strategy on inclusive education 2009 – 2017*. MoEST.

National Institute for Educational Development. (2016). *National curriculum for basic education.* Ministry of Education, Arts and Culture.

Nyerere J. K. (1967). *Education for self-reliance.* Government printer.

Persekutuan, P. P. K. (2013). *Malaysia education blueprint 2013-2025* (Preschool to Post-Secondary Education). Kementerian Pendidikan.

Tanzania Institute of Education. (2007). C*urriculum for ordinary level secondary education in Tanzania*. Tanzania Institute of Education.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2022). *Ripoti ya maoni ya wadau kuhusu uboreshaji wa mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu*. TET.

The United Republic of Tanzania. (2019). *National curriculum framework for basic and teacher education.* Ministry of Education, Science and Technology.

UNESCO. (1990). *Joemtien World Conference on EFA.* UNESCO.

United Republic of Tanzania. (1999). *The Tanzania development vision 2025*. United Republic of Tanzania.